**TAREHE 27 HADI 30 NOVEMBA 2023**

**LUSAKA, ZAMBIA**

# KONGAMANO LA 3 LA KIMATAIFA KUHUSU AFYA YA UMMA BARANI AFRIKA

**KUVUNJA MIPAKA: KUWEKA UPYA MSIMAMO WA BARA LA AFRIKA KWENYE MFUMO WA AFTA WA KIMATAIFA**

## CPHIA 2023 Muhtasari wa Uwasilishaji wa Matukio Madogo

Kongamano la 3 la Kimataifa kuhusu Afya ya Umma Barani Afrika (CPHIA, Conference on Public Health in Africa 2023) litakalofanyika kuanzia tarehe 27 hadi 30 Novemba jijini Lusaka, Zambia sasa linafungua kipindi cha kuwasilisha maombi ya kuandaa matukio madogo. Likiwa litaandaliwa katika kituo cha Mulungushi International Conference Center, kongamano la mwaka huu litaangazia jinsi bara hili linavyochochea ubunifu na utafiti wa kisayansi ili kuzalisha maarifa mapya na bidhaa mpya za afya.

Kwa kuendeleza msingi wa ufanisi wa kongamano la CPHIA 2022, ambalo liliangazia zaidi ya matukio 50 ya ana kwa ana na ya mtandaoni, washirika maalum wataalikwa ili kuandaa matukio madogo rasmi ya kongamano la CPHIA 2023. Matukio haya yatakuza mazungumzo yanayofanyika wakati wa kongamano, kuonyesha mbinu bora, kuhimiza hali ya kushiriki maarifa na kukuza ushirikiano wa wadau wengi. Mashirika kutoka kwenye sekta nzima ya afya ya umma yanaalikwa kutuma maombi. Maombi hayo yanapaswa kulingana na Mfumo Mpya wa Afya ya Umma wa Africa CDC, yakiangazia mada ambazo zinajumuisha kiwango cha kujiandaa na kushughulikia matukio ya dharura, utafiti na maendeleo, ubunifu, utengenezaji wa ndani wa bidhaa, bima ya afya ya jumla, afya na uongozi wa wanawake, ushirikishaji wa vijana na mashirika ya kijamii, ushirikishaji wa sekta ya kibinafsi, ushirikiano, magonjwa ya kuambukiza na zaidi.

Angalia hapa chini ili uone mwongozo na maelezo kuhusu jinsi ya kuwasilisha pendekezo la tukio dogo.

**Kipindi cha mwaliko wa kutuma maombi kitafungwa mnamo Ijumaa tarehe 11 Agosti: Tafadhali jaza na uwasilishe fomu ya maombi inayohitajika kufikia saa 23:59 CAT/21:59 UTC.**

**Tarehe ya kuarifiwa: Waandalizi wataarifiwa kuhusu hali ya pendekezo lao la tukio dogo kufikia Ijumaa, tarehe 1 Septemba 2023.**

Ukichaguliwa, timu ya kongamano la CPHIA 2023 itasaidia katika kubainisha wakati na mahali, na kukuunganisha na timu ya mipango ya huduma ili kupanga huduma za ziada, kama inavyohitajika.

## Mwongozo wa Kutuma Maombi

Waandalizi wanapaswa kuwasilisha lengo dhahiri la dhamira ya tukio lao ambalo linakamilishana na dhamira ya Africa CDC ya Mfumo Mpya wa Afya ya Umma. Wanapaswa pia kulenga kuwa na mkusanyiko wa wazungumza mbalimbali, ikijumuisha usawa thabiti wa jinsia na maeneo.

Ni idadi ndogo ya matukio madogo ambayo inaweza kuandaliwa kwenye ukumbi wa mkutano. Tutatoa nafasi kwa idadi nyingi iwezekanavyo. Uteuzi wa matukio madogo utakuwa kwa msingi wa ushindani. Waandalizi watarajiwa wa matukio madogo wanahimizwa wazingatie kushirikiana na mashirika mengine ambapo kuna mwingiliano wa dhamira sawa. Pia, tafadhali bainisha kwenye fomu ya maombi ikiwa utakuwa tayari kushirikiana na waombaji wengine wanaopendekeza tukio dogo kama lako.

**Limeandaliwa na:**

Republic of Zambia

Waandalizi wa tukio dogo wanatarajiwa kuhudhuria kongamano ana kwa ana na kutangaza tukio hilo kupitia mitandao yao. Matangazo yote ya tukio dogo na usimamizi wa wahudhuriaji pia ni jukumu la waandalizi wa tukio dogo.

Matukio madogo yataandaliwa siku nzima mnamo tarehe **27 Novemba**, na baadhi ya matukio madogo ya ziada yakiandaliwa asubuhi au jioni kuanzia tarehe **28 hadi 30 Novemba, kwa kutuma ombi**.

Mapendekezo ya matukio madogo ya mtandaoni yatazingatiwa. Tafadhali bainisha kwenye fomu ya maombi ikiwa ungependa kuandaa tukio lako dogo mtandaoni. Mwandalizi wa tukio dogo la mtandaoni atawajibika kwa mipango yote ya huduma, utangazaji na usimamizi wa wahudhuriaji. Matukio madogo ya mtandaoni yataandaliwa mnamo tarehe **27 Novemba** pekee.

## Masharti ya Kutuma Maombi

Ombi lako la kuandaa tukio dogo lazima lijumuishe yafuatayo:

- Kichwa cha tukio dogo linalopendekezwa.
- Maelezo ya tukio linalopendekezwa na jinsi linavyohusiana na dhamira ya Africa CDC ya Mfumo Mpya wa Afya ya Umma **(yasizidi maneno 250)**.
- Matokeo yanayotarajiwa kutokana na kipindi hicho **(yasizidi maneno 100)**.
- Idadi ya wageni wanaotarajiwa.

*Tafadhali kumbuka kuwa mawasilisho yanayozidi kikomo cha juu cha idadi ya maneno hayatazingatiwa.*

## Vifurushi vya Huduma za Matukio Madogo

Ada ya usajili wa matukio madogo ya kongamano la CPHIA 2023 ni Dola 2, 000 za Marekani (USD $2,000). Huduma za ziada zinapatikana kwa gharama ya ziada na huduma za chakula zinaweza kupangwa kando. Tafadhali bainisha huduma za ziada unazohitaji kwenye fomu ya matukio madogo.

Ili utusaidie tutimize mahitaji yako vyema, tafadhali bainisha kifurushi cha huduma utakazohitaji kwa ajili ya tukio lako na ikiwa unahitaji huduma yoyote ya ziada kando na huduma zinazotolewa hapa chini.

### Kifurushi cha 1: ($2,000)

- Chumba chenye ukubwa na viti vya kutosha idadi ya wahudhuriaji wanaotarajiwa
- Chupa za maji, kalamu na vijitabu vya madokezo kwa idadi ya wahudhuriaji wanaotarajiwa
- Mfumo wa vifaa vya sauti na picha, ikijumuisha maikrofoni mbili na uwezo wa kufikia mtandao wa WIFI
- Usaidizi wa kiufundi, kama inavyohitajika
- Huduma za tafsiri kwa lugha za Muungano wa Afrika
- Kuondolewa kwa ada ya usajili kwa mtu mmoja (mwandalizi mkuu wa tukio dogo)
- Kuorodhesha tukio dogo kwenye tovuti ya kongamano la CPHIA 2023 chini ya mpango wa matukio madogo rasmi

### Kifurushi cha 2: ($4,000)

Kinajumuisha huduma zote zilizo kwenye kifurushi cha 1 pamoja na:

- Kurekodi tukio
- Kutiririsha tukio moja kwa moja
- Kushiriki kwa njia ya mtandaoni kwa wazungumzaji wakuu
- Zaidi ya maikrofoni mbili
- Matangazo ya hali ya juu ya tukio dogo kwenye mitandao yote ya kongamano la CPHIA, ikijumuisha hadi machapisho 4 kwenye Twitter, IG na LinkedIn (wakati na maudhui vitapangwa kwa ushirikiano na timu ya mpango ya kongamano)